



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA SIKONGE



Banua zote zinazidhika na kutumwa kwa:

Tel: +255 262 965732 (Direct line)
+255 659 566703
e-mail: ded@sikongedc.go.tz
Tovuti: sikongedc.go.tz

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji (W)
Halmashauri ya Wilaya ya Sikonge
4 Mtaa wa Bomanji
S.L.P 70
45382 - SIKONGE TABORA

10/07/2023

**TANGAZO LA ZABUNI YA KUKODISHA CANTEEN (MGAHAWA)
MPYA KWA AJILI YA KUTOA HUDUMA YA CHAKULA ILIYOPO
KWENYE JENGO LA MAKAO MAKUU YA HALMASHAURI –
LGA/121/2023/2024/NC/03**

MARUDIO

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Sikonge anawatangazia Wazabuni /Makampuni / Wajasiliamali / Ushirika / Vikundi au Wananchi wenye uwezo wa kukodi Canteen mpya kwa ajili ya kutoa huduma ya Chakula iliyopo kwenye jengo la Makao makuu ya Halmashauri ya Wilaya ya Sikonge .

MASHARTI YA MWOMBAJI.

1. Mwombaji awe ni raia wa Tanzania
2. Mwombaji aambatishe kivuli cha Leseni ya Biashara
3. Mwombaji aambatishe kivuli cha utambulisho wa mlipa kodi (TIN) number
4. Mwombaji aambatishe kivuli cha taarifa za Kampuni (**Company Profile** kwa makampuni tu)
5. Awe amesajiliwa na GPSA kwa mkataba wa '**FOOD AND REFRESHMENTS'**
6. Mwombaji ataje kiasi cha fedha atakacholipa Halmashauri kwa mwezi (Malipo ya pango kwa mwezi) na malipo haya yatafanyika kila mwanzo wa mwezi (kabla ya kuanza kazi) katika mwezi husika kwa kuchukua 'Control number' toka Ofisi ya Idara ya Fedha
7. Mwombaji atakayepata kazi hii atawajibika kulipia bili ya umeme na maji kulingana na atakavyoelekezwa na Halmashauri
8. Gharama za Usafi kwenye eneo la biashara ni jukumu lake mwenywewe

9. Mwombaji awe na vyombo vya kutosha kufanya kazi
10. Mwombaji awe na vitendea kazi mwenyewe kama viti, meza, kabati za kuhifadhi chakula nk.
11. Mwombaji ataje uzoefu na sifa zake zote katika maombi ya kazi anayoomba
12. Endapo Mwajili hataridhika na mwenendo wa huduma inayotolewa na Mzabuni atasitisha mkataba wakati wowote.
13. **Mwombaji atakayepata kazi hii ahakikisho Wafanyakazi wake wana vyeti vya kupima Afya (Medical Examination Certificate).**


MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA KWA WAOMBAJI WOTE WENYE SIFA NI KAMA IFUATAVYO;

- i. Mwaombaji anatakiwa kulipia Kitabu cha Zabuni kwa kazi aliyoomba kiasi cha Tsh. 30,000/= baada ya kupewa Bill / Control number / Account number toka Ofisi ya Mwekahazina / Uhasibu. Kitabu cha zabuni kinapatikana katika Ofisi ya Manunuzi na Ugavi (PMU). **Risiti original aliyolipia mwombaji iambatanishwe kwenye barua yake ya maombi.**
- ii. Mwombaji aandike jina na namba ya kazi aliyoomba juu ya bahasha ya maombi na atatoa NAKALA MOJA ya kitabu cha maombi na kitabu kimoja ORIGINAL vyote vifungwe kwenye bahasha moja na kuandikwa JINA na NAMBA YA ZABUNI husika juu ya bahasha ya maombi
- iii. Barua ya Maombi iandikwe kwenda anwani ifuatayo;
KATIBU BODI YA ZABUNI,
S.L.P 70,
SIKONGE.

14. Siku ya mwisho ya kuwasilisha maombi ni tarehe 24/07/2023, Jumatatu saa 5.00 asubuhi na ufunguzi utafanyika mara baada ya muda wa mwisho wa kuwasilisha maombi katika ukumbi wa mikutano wa Halmashauri.

Waombaji au Wawakilishi wao wanakaribishwa kuhudhuria ufunguzi wa maombi yao. Baada ya ufunguzi taratibu zingine za Manunuzi zitafuata.

Imetolewa na;


Seleman M. Pandawe
Mkurugenzi Mtendaji (W)
SIKONGE

MKURUGENZI MTENDAJI
WILAYA - SIKONGE.